



Feed the Future Tanzania Mboga na Matunda (FTFT-MnM)

Muda wa Mradi

Januari 2017 – Juni 30, 2022

Bajeti

Dola za Marekani milioni 24.9

Maeneo ya Mradi

Zanzibar na Mikoa ya Morogoro, Iringa, Mbeya na Songwe iliyopo katika Mpango wa Kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT).

Watekelezaji

Fintrac Inc.

Mawasiliano: Antonio Coello
(antonio@fintrac.com)

Washirika

Tanzania Horticulture Association (TAHA) na Wadau wa Sekta Binafsi

Mawasiliano ya USAID

Judith Kitivo (jkitivo@usaid.gov)



Wakulima wa Kikundi cha Hapa Kazi wakionesha maboga yaliyozalishwa kwa mwongozo kutoka kwa Mtaalam wa Kilimo wa Mradi na Afisa Ugani wa Serikali..

Wakulima wadogo wa kilimo cha mazao ya bustani nchini Tanzania hukabiliwa na changamoto kadhaa. Ufinyu wa upatikanaji wa masoko ya ndani na ya nje ni kikwazo, kutokana na mifumo duni na isiyo na mpangilio mzuri ya soko la mazao ya bustani. Uzalishaji duni kwa wakulima wadogo hupunguza tija, na fursa; na huduma za ugani za kilimo za sekta ya umma hazikidhi kuleta ufanisi wa stadi za biashara au teknolojia bora kwa wakulima. Wanawake na vijana hukabiliwa na changamoto ngumu zaidi: hususani upatikanaji wa ardhi, fedha na pembejeo bora za kilimo.

Madhumuni ya mradi wa *Feed the Future Tanzania Mboga na Matunda* ni kufanya sehemu ndogo ya kilimo cha mazao ya bustani iwe na ushindani zaidi na jumuishi pamoja na kuboresha hali ya lische ya Watanzania kwa:

- Kuongeza teknolojia zilizoreshwa na mbinu za kuongeza tija kwa wakulima wadogo, kwa kuhusisha idadi kubwa ya wanawake na vijana katika bidhaa lengwa.
- Kupanua mifumo ya soko inayoweza kufikia idadi kubwa ya walengwa wa moja kwa moja na wasio wa moja kwa moja, kwa kuzingatia wenye uhitaji zaidi, na kuongeza biashara kwa bidhaa lengwa.
- Kuimarisha uwezo wa jumla wa tasnia ya kilimo cha mazao ya bustani.



MKAKATI

Mradi hutumia mbinu za mifumo ya soko na kushirikisha wadau katika kutoa huduma na miongozo bora ya kilimo, ujuzi wa uboreshaji biashara, teknolojia za msingi, na elimu ya lishe kwa walengwa zaidi ya 700,000. Mbinu za utekelezaji huhimiza kupokea ujuzi na ubunifu katika ngazi ya mkulima, na mbinu bora za biashara katika ngazi ya soko, ili kutoa manufaa kwa upana zaidi.

Hata hivyo mradi hutumia mikakati jumuishi ili kuongeza ushiriki na manufaa zaidi kwa wanawake na vijana katika tasnia ya kilimo cha mazao ya bustani; ikiwa ni pamoja na mikakati inayowezesha upatikanaji rahisi wa ardhi, huduma za kifedha, na taarifa za soko ili kuzalisha mapato kwa kaya za vijijini pamoja na kupanua wigo wa uzalishaji wa mazao yenye lishe.

Ili kukuza ushindani endelevu wa tasnia ya kilimo cha mazao ya bustani, mradi hufanya kazi na wajasiriamali wadogo na wa kati zaidi ya 2,500 (MSMEs), maafisa ugani wa serikali 200, na wadau wengine zaidi ya 20; kuongeza tija kwa wakulima wadogo, na faida katika mnyororo mzima wa soko na kilimo cha mazao ya bustani.

MATOKEO YA MRADI

- Mradi umenufaisha zaidi ya watu 724,000 kati yao asimia 58 ni vijana na asilimia 45 ni wanawake.
- Katika Mwaka wa Fedha 2020, karibu walengwa 677,000 walipokea mbinu na teknolojia bora katika hekta zaidi ya 421,000. Kupokea teknolojia mpya kumeongeza wastani wa mavuno ya mazao muhimu (nyanya, kabichi, vitunguu, viazi ulaya, tikiti maji, na pilipili tamu) takribani kwa asilimia 37.
- Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, zaidi ya dola milioni 80 zimewekezwa na wadau wa sekta binafsi wanaofanya kazi na mradi na kuzalisha mauzo ya bidhaa na huduma za zaidi ya dola milioni 260. Kati ya mauzo hayo, asilimia 31 ni kutoka kwa wakulima wadogo (dola milioni 79.5).
- Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, mradi umewezesha upatikanaji wa zaidi ya dola milioni 7.9 za mikopo na kunufaisha wadau wa mnyororo wa thamani zaidi ya 5,200.
- Hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2020, zaidi ya wakulima 16,600 walikuwa wakizalisha kibiashara mazao yenye lishe kwa wingi na mauzo yalifikia zaidi ya dola milioni 9.9.